



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA  
MAZINGIRA**

**TANGAZO KWA UMMA KWA WENYE VIWANDA VYA KUTENGENEZA  
BIDHAA ZA PLASTIKI KUSAJILI VIWANDA VYAO KWENYE BARAZA LA  
TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepewa jukumu la kuhakikisha mazingira na afya ya binadamu inalindwa. Kulingana na Kifungu cha 81 cha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, kinaelekeza wawekezaji wote kuhakikisha wanafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa shughuli zao za uwekezaji.

Kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji mkubwa wa bidhaa za plastiki nchini na uchafuzi wa taka hizi za plastiki kuongezeka kwenye mazingira, Baraza linachukua hatua shirikishi kwa wenye viwanda kwa kuwaagiza wamiliki wote wenye viwanda vya kutengeneza bidhaa za plastiki kuhakikisha ndani ya kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe 24 Aprili, 2023, wanasajili viwanda vyao na kutoa taarifa za kina kuhusiana na shughuli zao kwenye Ofisi za Baraza Makao Makuu Dodoma au katika ofisi Kanda zilizopo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Mtwara na Morogoro. Taarifa zinazohitajika kwenye usajili ni pamoja na;

- 1) Jina la kiwanda na umiliki wa kisheria wa kiwanda hicho;
- 2) Eneo kiwanda kilipo (Mkoa, Wilaya, Kata na Mtaa);
- 3) Aina ya bidhaa zinazozalishwa na uwezo wa kiwanda hicho kuzalisha aina hiyo ya bidhaa;
- 4) Malighafi zinazotumika kwenye uzalishaji wa bidhaa hizo na mahali zinakoagizwa;
- 5) Majina ya wanunuzi wakuu wa bidhaa zinazozalishwa na kiwanda;
- 6) Nakala za cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira au cheti cha Ukaguzi wa Mazingira. Kwa viwanda ambavyo havina vyeti husika vya mazingira, vinatakiwa kusajili kwenye Ofisi za Baraza ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kumbuka ni kosa la kisheria kuendesha shughuli za uwekezaji pasipo kuwa na cheti cha mazingira kulingana na Kifungu cha 184 cha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Baada ya muda uliotolewa kwisha, Baraza litaendesha ukaguzi nchi nzima kwa viwanda vyote vinavyozalisha bidhaa za plastiki. Baraza linawaelekeza wenye viwanda wote nchini kutimiza matakwa ya sheria pasipo shuruti.

***Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu  
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira  
24 Aprili, 2023***